**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**

# HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO, MHESHIMIWA DKT. PHILIP I. MPANGO (MB), KATIKA UZINDUZI WA MPANGO WA PILI WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO 2016/17 – 2020/21

**DODOMA**

**7 JUNI, 2016**

***Mheshimiwa Kassim M. Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;***

***Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;***

***Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;***

***Mheshimiwa Jaji Mohamed Chande Othman, Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;***

***Mheshimiwa George Masaju, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;***

***Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri;***

***Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;***

***Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma;***

***Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu;***

***Washirika wa Maendeleo;***

***Wageni Waalikwa;***

***Wanahabari;***

***Mabibi na mabwana.***

**1.** ***Mheshimiwa Waziri Mkuu,*** awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika siku ya leo ambayo ni muhimu na ya kihistoria tukiwa na afya njema ili tuweze kushuhudia uzinduzi wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2016/17 – 2020/21. Tuko hapa siku ya leo katika mwendelezo wa kutoa mwongozo wa maendeleo kwa nchi yetu ambao utaweka mikakati ya utekelezaji inayolenga kujenga msingi wa uchumi wa viwanda na maendeleo ya watu kwa kuhakikisha kuwa rasilimali na fursa za nchi zinatumika vizuri katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Hii ni katika utekelezaji wa azma ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya kufikia hadhi ya nchi ya uchumi wa kipato cha kati ifikapo 2025.

**2.** ***Mheshimiwa Waziri Mkuu,*** naomba uniruhusu niseme machache kuhusu Mpango ambao utauzindua hii leo.

**3.** ***Mheshimiwa Waziri Mkuu,*** Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango Elekezi wa Miaka 15 wa utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 uliozinduliwa mwaka 2012. Kwa mujibu wa Mpango Elekezi, dhima ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ilikuwa "*kujenga msingi wa uchumi wa viwanda*". Aidha, mwaka 2015, Serikali ilifanya uamuzi wa kuunganisha mifumo ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Mkakati wa Kukuza Uchumi na

Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA) katika mfumo mmoja jumuishi ili kuwianisha agenda ya kupunguza umaskini katika Mipango ya Maendeleo ya Taifa, na kuwa na mfumo mmoja wa utekelezaji.

**4.** ***Mheshimiwa Waziri Mkuu,*** kwa kuzingatia maamuzi hayo ya Serikali, dhima ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano imebadilika kutoka ile iliyobainishwa katika Mpango Elekezi na kuwa *"Kujenga Uchumi wa Viwanda ili Kuchochea Mageuzi ya Uchumi na Maendeleo ya Watu".* Uamuzi huu unalenga kutoa msukumo katika juhudi za Serikali kuchochea kasi ya ukuaji na mageuzi ya uchumi; kupunguza umaskini; na maendeleo ya watu.

**5.** ***Mheshimiwa Waziri Mkuu,*** naomba uniruhusu niwapongeze wataalam wa Tanzania kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Taasisi ya Utafiti wa Kupunguza Umaskini (REPOA) kwa mchango wao mkubwa na kushiriki kikamilifu katika maandalizi ya Mpango huu. Mfano huu mzuri ni wa kuigwa katika uandaaji wa Mipango na mikakati mbalimbali ya maendeleo kwa nchi yetu.

**6.** ***Mheshimiwa Waziri Mkuu,*** Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano una maeneo manne ya kipaumbele. Eneo la kwanza ni **kukuza uchumi na ujenzi wa msingi wa uchumi**

**wa viwanda** ambalo linajumuisha uzalishaji, ikiwa ni pamoja na sekta za kilimo, viwanda, madini na utalii. Eneo la Pili ni **Kufungamanisha Maendeleo ya Uchumi na Maendeleo ya Watu ambalo** linahusisha kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu (kuanzia malezi na elimu ya awali, elimu bora kwa wote, na fursa za kujiendeleza kitaaluma na ujuzi) kumwezesha mtu kujiajiri au kuajiriwa, kuimarisha na kuboresha afya ya mwananchi kama vile huduma za afya, usalama wa chakula na lishe, maji safi na mazingira safi ya kuishi, na hifadhi ya jamii.

**7.** ***Mheshimiwa Waziri Mkuu,*** eneo la tatu ni **kujenga mazingira wezeshi kwa uendeshaji biashara na uwekezaji**. Katika eneo hili, Mpango unalenga kuendelea kuimarisha miundombinu na huduma za msingi kwa uwekezaji, ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa nishati ya umeme, miundombinu ya reli, barabara, bandari, usafiri wa anga, usafiri wa majini, maji na TEHAMA. Eneo la nne ni **Kuimarisha Usimamizi wa utekelezaji wa Mpango.** Eneo hili ni mahsusi kwa lengo la kutanzua vikwazo vya utekelezaji na kuimarisha usimamizi, ufuatiliaji na tathmini ya Mpango.

**8.** ***Mheshimiwa Waziri Mkuu,*** katika Mpango huu, baadhi ya miradi ya kipaumbele imepewa sifa ya kuwa miradi ya kielelezo *(flagship projects)*. Miradi hii ni: mradi wa Makaa ya Mawe

Mchuchuma, mradi wa Chuma Liganga, Maeneo Maalum ya Uwekezaji, kituo cha Biashara na Huduma Kurasini, ujenzi wa Reli ya Kati na matawi yake kwa Kiwango cha *Standard Gauge* na ufufuaji wa Shirika la Ndege la Taifa (ATCL).

**9.** ***Mheshimiwa Waziri Mkuu,*** utekelezaji wa Mpango huu utafanikisha: kuimarika kwa kasi na ukuaji mpana wa uchumi kwa manufaa ya wananchi walio wengi ambapo uchumi unatarajiwa kukua kutoka asilimia 7.0 mwaka 2015 hadi asilimia 10 mwaka 2020; kuongeza kasi ya kupunguza umaskini ambapo Pato la wastani kwa kila mwananchi litaongezeka kutoka Dola za Kimarekani 1,006 mwaka 2015 hadi 1,500 mwaka 2020; kuongeza fursa za ajira kwa wote, hususan vijana na akina mama; kuongeza upatikanaji na ubora wa huduma za jamii; kubadili mfumo wa biashara kwa kuongeza mauzo nje ya bidhaa za viwandani badala ya kuuza bidhaa ghafi na wakati huo huo kulinda hifadhi ya mazingira.

**10.** ***Mheshimiwa Waziri Mkuu,*** utekelezaji wa Mpango huu utategemea zaidi ushiriki mkubwa wa Sekta Binafsi katika utekelezaji. Shilingi trilioni 107 zitahitajika katika utekelezaji wa Mpango na miradi ya maendeleo kwa kipindi cha miaka mitano. Serikali itachangia shilingi trilioni 59, sawa na wastani wa shilingi trilioni 11.8 kila mwaka. Wakati huo huo, sekta binafsi na washirika

wa maendeleo wakichangia shilingi trilioni 48, sawa na shilingi trilioni 9.6 kwa mwaka.

**11.** ***Mheshimiwa Waziri Mkuu,*** Mpango huu utatekelezwa kupitia Mpango wa Maendeleo wa kila mwaka ambapo vipaumbele vya kila mwaka vitaainishwa na kutekelezwa kwa kujenga msingi wa uendelezaji katika miaka inayofuata. Vile vile, ufuatiliaji na tathimini ya utekelezaji wa Mpango huu utafanyika na kutoa taarifa katika ngazi zote stahiki.

**12.** ***Mheshimiwa Waziri Mkuu,*** baada ya maelezo hayo mafupi kuhusu Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano, nakuomba sasa utupe nasaha zako na hatimaye uzindue rasmi Mpango huu.

**13.** ***Mheshimiwa Waziri Mkuu,*** Karibu Sana.